
# AFISI YA MWANASHERIA MKUU

## HISTORIA YA AFISI YA MWANASHERIA MKUU KABLA YA MAPINDUZI YA 1964



Jengo Baada ya Mapinduzi hadi 2013

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni kati ya afisi kongwe iliyoanzishwa na wakoloni mnamo mwaka 1913-1914 wakati Utawala wa Kikoloni walipoweka Mahamia ya Kikoloni hapa Zanzibar. Afisi hii wakati ilipoanzishwa ilikuwa na kazi ya kutoa ushauri kwa Serikali na kutekeleza masuala yote ya kisheria kwa niaba ya Serikali.

Kwa kipindi hicho Mwanasheria Mkuu alikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria na Utawala (Executive and legislative Council) la mwaka 1926. Baraza hili kazi yake kuu ilikuwa ni kutunga sheria na kumshauri Sultan katika masuala ya utawala. Aidha, Mwanasheria Mkuu aliendelea kufanya kazi zake hata katika Baraza la Kutunga Sheria na Utawala la mwaka 1936 na alikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza hili lililodumu hadi Mapinduzi ya mwaka 1964.

## BAADA YA MAPINDUZI YA 1964




Jengo la Sasa kuanzia 2013

Baada ya Mapinduzi ya 1964, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliendelea kuwepo na kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria ikiwa ni pamoja na kusimamia kesi za jinai. Baada ya Mapinduzi Mwanasheria Mkuu hakuwa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi ambalo lilikuwa na kazi ya kumshauri Rais na kutunga Sheria tofauti na kipindi cha ukoloni na hali ya sasa ya kuwa Mwanasheria Mkuu ni mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Baraza la Wawakilishi.

Kimsingi nafasi ya Mwanasheria Mkuu imeanzishwa na kutambuliwa na Katiba ya Zanzibar 1984 chini ya kifungu cha 55 (1) ambacho kinaeleza: “Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ambaye ni Mzanzibari na ambaye atateuliwa na Rais”. Kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar 1984 kinaeleza kazi za Mwanasheria Mkuu na kimeeleza: “Mwanasheria Mkuu ndiye atakuwa Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na atatekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitakapopelekwa kwake au atakazopangiwa na Rais au kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria nyenginezo zozote”.

Kwa sasa kazi na majukumu ya Mwanasheria Mkuu yameongezeka kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kisiasa. Kazi hizo na majukumu yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013.